

Puffers and Spacers (Swahili)

Pufa na vifaa vya kupeana dawa (spacers)



Pufa ni nini?

Pufa (au kivuta pumzi) hutumiwa kutibu dalili za kupumua (sauti ya juu ya mluzi wakati wa kuvuta na kutoa pumzi).

Pufa zinaweza kuwa dawa za kutuliza (huondoa dalili, kurahisisha kupumua) au dawa za kuzuia (huzuia dalili kurudi).

Kifaa cha kupeana dawa ni nini?

Kifaa cha kupeana dawa (spacer) ni kifaa chenye umbo la silinda kinachounganishwa na pufa. Kwa kawaida, utachukua nyumbani spacer (na maski, inapohitajika) ambayo mtoto wako alitumia hospitalini. Unaweza kununua vifaa vya kupeana dawa kutoka kwa maduka ya dawa ya mtaa.


Wakati wa kutumia kifaa cha kupeana dawa

Watoto wote wanapaswa kutumia kifaa cha kupeana dawa kuvuta (kupumua) dawa zao za pufa. Kifaa cha kupeana dawa hupunguza kiasi cha dawa kinachoringia kwenye kinywa cha mtoto wako, hivyo zaidi inaweza kusafiri hadi kwenye mapafu.

Jinsi ya kutumia kifaa cha kupeana dawa (spacer)


Hatua ya 1

Ondoa kifuniko kutoka kwa pufa (na kifaa cha kupeana dawa ikiwa kuna moja). Shikilia pufa wima na utikise vizuri.



Hatua ya 2

Ambatisha pufa kwenye mwisho wa kifaa cha kupeana dawa.




Hatua ya 3

Weka mdomo wa spacer kwenye mdomo wa mtoto.

Hatua ya 4

Toa pumzi moja ya dawa kwenye kifaa cha kupeana dawa na umwombe mtoto wako apumue ndani na nje kwa kawaida kwa pumzi 4.



Hatua ya 5

Tikisa pufa na kifaa cha kupeana dawa kati ya kila dozi. Rudia kumpa mtoto wako idadi ya dozi kama alivyoshauriwa na daktari wako. Weka kifuniko tena kwenye pufa unapomaliza.



Ninapaswa kutumia maski pamoja na kifaa cha kupeana dawa lini?

Ikiwa mtoto wako hawezi kuziba kifaa cha kupeana dawa kwa midomo yake, anapaswa kutumia maski. Aina ya maski itatofautiana kulingana na ukubwa wa uso wa mtoto.


Jinsi ya kutumia maski na kifaa cha kupeana dawa

Hatua ya 1

Ambatanisha maski kwenye mdomo wa kifaa cha kupeana dawa (na pufa iliyoambatanishwa).

Hatua ya 2

Weka maski kwa upole kufunika mdomo na pua ya mtoto wako na hakikisha kuwa hakuna mapengo.



Hatua ya 3

Toa pumzi moja ya dawa kwenye kifaa cha kupeana dawa. Shikilia spacer na maski kwenye mahali pao wakati mtoto wako anapumua ndani na nje kwa pumzi 4.

Hatua ya 4

Tikisa pufa na kifaa cha kupeana dawa kati ya kila dozi. Rudia kumpa mtoto wako idadi ya dozi zinazohitajika. Weka kifuniko tena kwenye pufa unapomaliza.

Kusafisha kifaa cha kupeana dawa

Osha spacer katika maji ya joto yenye sabuni kabla ya matumizi ya kwanza na kila mwezi baada ya hayo. Usisuuze. Tikisa mabli maji yoyote na uiache ili hewa ikauke. Usikaushe kifaa cha kupeana dawa na kitambaa au karatasi ya kukaushia. Muuguzi wa mtoto wako, daktari, mwalimu wa pumu au mfamasia anapaswa kuangalia spacer kila baada ya miezi 6 hadi 12.

Imeandaliwa na Idara ya Dharura, Hospitali ya Watoto ya Queensland. Tunatambua mchango wa watumiaji na walezi.

Resource ID: FS092 **Reviewed:** July 2022

Kanusho: Maelezo haya yametolewa na wataalamu wa afya kama mwongozo pekee na yanalenga kusaidia, si kubadili nafasi, majadiliano na daktari wa mtoto wako au wataalamu wa afya. Taarifa husasishwa kila mara, kwa hivyo tafadhali angalia kuwa unarejelea toleo la hivi majuzi zaidi. Tafuta ushauri wa matibabu, inapofaa, kwa wasiwasi kuhusu afya ya mtoto wako.